HakiElimu
Education Brief Na.07.1K

# Kufuatilia Fedha za Elimu

## Kiasi gani hutumika kwa Elimu?

Kupanua upatikanaji wa elimu ya msingi na sekondari kumekuwa kipaumbele dhahiri katika miaka ya hivi karibuni. Katika hotuba ya bajeti 2007/08 iliyotolewa Bungeni, tarehe 14 June, 2007 Waziri wa Fedha aliibainisha elimu kama sekta ambayo itapata kiasi kikubwa zaidi cha fedha – *zaidi ya shilingi trilioni moja* - au 18% ya matumizi yote.[i]




## Fedha zinatoka wapi?

Rasilimali za Serikali kwa ajili ya elimu zinatokana na mapato ya ndani na ya nje. Zamani, fedha za wafadhili kwa ajili ya elimu zilielezwa bayana zaidi, kupitia mfuko wa jumla wa sekta ya elimu na taratibu nyingine zilizokuwa za wazi zaidi. Hata hivyo, mabadiliko ya sasa kuelekea msaada wa bajeti ya jumla, yanamaanisha kwamba wabia wa maendeleo wanatoa fedha nyingi zaidi moja kwa moja Serikalini, ambayo nayo baadaye huamua jinsi ya kuzigawa kwenye vipaumbele mbalimbali, ikiwemo elimu. Hili hufanya iwe vigumu kuamua kwa uhakikia kiasi gani cha bajeti kinagharimiwa na wafadhili.[ii]

## Nani husimamia elimu?[iii]

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ni kiini cha midahalo mingi inayozungukia sera ya elimu. Hata hivyo, Wizara ya Elimu husimamia chini ya nusu ya bajeti ya elimu.[iv] Wizara na idara nyingine kadhaa zinahusika, zikiwemo Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Elimu ya Juu, Sanyansi, na Teknolojia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Wizara ya Fedha na sekretariati 21 za mikoa.

Mojawapo ya sababu kuu za kujihusisha kwa vyombo hivi mbalimbali ni kwamba sehemu kubwa ya wajibu kwa elimu ya msingi imegatuliwa kwa ngazi ya Serikali za Mitaa. Wakati ambapo Wizara ya Elimu inaendelea kuelekeza sera ya elimu, sehemu kubwa ya fedha za elimu ya msingi imekusudiwa kuwa chini ya mamlaka ya TAMISEMI na mikoa.[v] Hata hivyo, hakuna utaratibu wa kukusanya taarifa za bajeti kwa ajili ya sekta nzima. Jambo hili linaleta kikwazo kikubwa kwenye ugawaji wa kimkakati wa rasilimali.[vi]

## Mambo gani Huunda Bajeti?

Mipango sambamba na michakato ya utengenezaji wa bajeti hufanya iwe vigumu kufuatilia fedha za elimu. Upangaji mipango wa kuanzia chini kwenda juu na michakato ya uandaaji wa bajeti huanzia kwenye ngazi ya kijiji na, hatimaye, huelekea kwenye bajeti iliyopitishwa kwenye ngazi ya Halmashauri ya Wilaya. Wakati huohuo, upangaji mipango unaoanzia juu kwenda chini na michakato ya uandaaji wa bajeti huanzia kwenye ngazi ya Wizara ya Serikali Kuu, vikisababisha bajeti nyingine rasmi iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na kupitishwa na Bunge. Ngazi hizi mbili – hazikufungamana na hazikupatanishwa vizuri. Bajeti tofauti zinazotokeza zinaleta mchanganyiko na kuzuia utekelezaji wa ulipaji wa wakati muafaka. Zaidi ya hayo, wilaya na shule hupokea fedha zenye utondoti wa shuruti na maelekezo ya jinsi ya kuzitumia, jambo ambalo mara nyingi halipatani na mipango na vipaumbele vya mahali.

## Je, fedha hutiririkaje?

Fedha kwa ajili ya elimu hutumika kwenye ngazi mbalimbali na wizara za Serikali kuu (Wizara ya Elimu, TAMISEMI) pamoja na wakala wenye majukumu ya mitihani (NECTA) na mtaala (TIE), na halafu kwenye ngazi za mkoa, wilaya na shule. Idadi ya ngazi mbalimbali na vyombo vya Serikali vinavyohusika ina maana mara nyingi kuna njia nyingi za kugharimia jambo hilohilo. Kwa mfano, wilaya hupokea fedha kwa ajili ya ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi (ambayo hutoa fedha kwa ajili ya vitabu na vifaa vinginenvyo vya kufundishia na kujifunzia) kutoka kwenye uhamisho wa Ruzuku ya Jumla ya Elimu ambayo hupitia Wizara ya Fedha na TAMISEMI. Wilaya pia zimepokea fedha za ziada kwa ajili ya ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi moja kwa moja kutoka Wizara ya Elimu katika miaka ya hivi karibuni.[vii]

Kwa kiasi fulani, ugharimiaji wa elimu ya ya sekondari uko wazi, kwani fedha zimehamishwa moja kwa moja kutoka Wizara ya Elimu kwenda shule za sekondari. Hata hivyo, hili mara nyingi huziacha gizani Halmashauri za Serikali za Mitaa.

Ukiacha hizi njia kuu mitiririko mingine ya kifedha haina mipaka bayana kwa ajili ya elimu lakini bado ni vyanzo muhimu vya kugharimia sekta hii. Kwa

mfano, Ruzuku ya Mtaji wa Maendeleo wa Serikali za Mitaa (LGCDG) ni uhamisho kwa wilaya stahilifu[viii] wa mtaji wa uwekezaji katika miundombinu mipya na ukarabati mpya. Fedha za LGCDG zinaweza kutumika kwa mambo mbalimbali kwa busara ya wilaya lakini hadi leo, kwa kiasi kikubwa, zimekuwa zikitumika kwa miundombinu ya shule.

**Mtiririko wa Fedha za Elimu ya Msingi na Sekondari**




Zaidi ya hapo, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo la Uchaguzi (CDF), unaotazamiwa kuanzishwa 2007, utampa kila Mbunge kiasi fulani cha fedha za umma zilizotengwa kutumiwa kwenye miradi katika jimbo lake la uchanguzi. Huu unaweza kuwa chanzo kingine cha fedha kwa ajili ya miundombinu ya shule.

Mwisho, kuna fedha za "nje ya bajeti", kama vile Mfuko wa Kusaidia Jamii Tanzania (TASAF), ambao hutoa ruzuku za hiari kwa wilaya kwa ajili ya kujenga au kuboresha miundombinu ya kivitu. Hadi hivi sasa kiasi kikubwa cha fedha za TASAF kimetumika kwa miundombinu ya kielimu.[ix] Juhudi nyingine zinazogharimiwa na wafadhili na AZISE pia huhamishia rasilimali moja kwa moja shuleni.

Kama ilivyooneshwa kwenye programu hapo juu, mfumo huu tata hufanya iwe vigumu sana kufuatilia fedha za elimu.

## Hitimisho

Elimu ni kipaumbele dhahiri katika bajeti ya 2007/08, na sekta hiyo inaelekea kuwa tayari kupokea ongezeko kubwa katika rasilimali. Hata hivyo, kwa kuzingatia utata wa mchakato wa bajeti ya elimu, haiko bayana iwapo ongezeko hili litakuwa na maana ya kuongeza ubora wa elimu. Mapendekezo haya hapa chini yanaweza kuhakikisha kwamba ongezeko katika fedha litakuwa na athari kubwa.

## Kifanyike nini?

1. ***Rahisisha mchakato wa bajeti ya elimu***
   Kunapaswa kuwepo na mfumo mpana zaidi kwa ajili ya kugharimia elimu. Yaani – chanzo kikuu kimoja cha fedha, mpango mkuu mmoja (bajeti) kwa ajili ya kutumia fedha hizo, na taarifa kuu kuhusu jinsi fedha zilivyotumika.

2. ***Ubayana wa wajibu na Majukumu***
   Mgawanyo wa wajibu na majukumu kati ya Wizara mbalimbali uwe bayana na wa kimantiki. Wizara ya Elimu iongoze sera na iratibu vitu kama vile mitihani ya wanafunzi na mafunzo ya ualimu kabla ya kazi. Kwa kuzingatia hatua za kugatua elimu, TAMISEMI iwe chanzo cha fedha zote zinazotumika kwenye ngazi ya shule.

3. ***Ongeza uwazi***
   Taarifa za bajeti ya elimu zitolewe katika namna iliyo wazi na inayoeleweka ili wazazi na Walimu wawe na uwezo wa kufuatilia. Tabia ya sasa ya kuchapisha uhamisho katika magazeti inastahili kusifiwa, lakini matangazo haya yanapaswa yawe mapana zaidi na kutoa maelezo zaidi. Taarifa hizi pia zingeweza kutolewa kupitia vyombo vinavyotumika zaidi kama vile matangazo ya redio na TV, na pia yangeweza kuwekwa kwenye mbao za matangazo za shule.

---

i *Tarakimu za bajeti ya mwaka uliopita zilizooneshwa kwenye jedwali zimetolewa kwenye mafanikio ya Bajeti ya 2006/07*

ii *Kwa ujumla, fedha za wafadhili (zikijumlisha msamaha wa madeni) zinaoneshwa kuchangia 42% ya bajeti yote katika 2007/08, kwa mujibu wa Hotuba ya Bajeti.*

iii *Muhtasari huu unarejea Tanzania Bara tu. Mfumo wa Elimu wa Zanzibar ni tofauti kabisa na haufikiriwi hapa*

iv *Kwa msingi wa makadirio ya bajeti ya 2007/08 kwa Wizara ya Elimu kwa kulinganisha na mgao wote wa sekta uliotamkwa katika hotuba ya bajeti.*

v *DEGE Consult (2007), "Study on Local Level Service Delivery, Decentralisation and Governance for JICA"*

vi *2007 Public Expenditure and Financial Accountability Review (PEFAR) (World Bank)*

vii *Miongozo ya Bajeti ya Serikali za Mitaa, 2007/08 (TAMISEMI)*

viii *Shuruti hizi zimekusudiwa kuonesha uwezo wa wilaya kutekeleza vizuri miradi ya maendeleo, kutoa gharama kufanana na kutoa maelezo ya matumizi ya fedha. Kwa mfano, wilaya hazistahili kupata fedha hizi iwapo zinapata maoni mabaya kutoka kwa mdhibiti na mkaguzi Mkuu. (Chanzo: Miongozo ya Bajeti ya Serikali za Mitaa, 2007/08)*

ix *N.M. Lenneiye, (2005) "Who has the yam, and who has the knife: Social Action Funds and decentralization in Malawi, Tanzania, and Uganda", Social Protection Discussion Paper No. 0518, Social Protection Network, World Bank.*

---

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

hakielimu